

Hati ya maelezo muhimu - Amri ya Usalama wa Jumuiya ya Shule

Je, Amri ya Mara Moja ya Usalama wa Jumuiya ya Shule ni nini?

Baadhi ya watu, kama vile walimu wakuu wa shule na wafanyakazi wa Idara ya Elimu na Mafunzo, wanaitwa ‘watu walioidhinishwa’. Wana uwezo wa kutoa Amri ambazo zinakuwekea sheria za kufuata unapoenda au kuingiliana na shule.

Amri hukuzuia kuingia au kukaa kwenye uwanja wa shule au maeneo mengine ambapo shughuli za shule hufanyika. Amri inaweza kujumuisha maelezo kama vile nyakati, au maeneo ambayo Amri haitumiki.

Maelezo zaidi kuhusu Amri za Usalama wa Jumuiya ya Shule yanaweza kupatikana [hapa](#). Unaweza kutazama video [hapa](#) ili kukusaidia uelewe kile ambacho Amri za Usalama wa Jumuiya ya Shule hufanya.

Amri ya Mara Moja hudumu kwa muda gani?

Amri pia inakuambia ni muda gani sheria hizi zitatumika. Muda mrefu zaidi ambao Amri inaweza kuwekwa ni siku 14.

Ikiwa nina mtoto shuleni, ataathirika vipi kwa sababu sasa ninahitajika kufuata Amri ya Mara Moja?

Shule yako imezingatia kwa makini jinsi Amri itakavyoathiri mtoto wako na jinsi unavyomtunza. Amri haikusudii kukuzuia kumtunza au kujihusisha na elimu yake.

Shule yako itakupa ‘Itifaki ya Mawasiliano na Ufikiaji’ haraka iwezekanavyo baada ya kukupa Amri. Hii itaeleza:

- jinsi unavyoweza kujulishwa kuhusu elimu ya mtoto wako
- jinsi mtoto wako anavyoweza kuendelea kwenda shule na kushiriki katika shughuli za shule kwa usalama
- watafanya nini ili kuhakikisha mtoto wako anasaidiwa na kutunzwa.

Je, nifanye nini ikiwa sikubaliani na Amri ya Mara Moja?

Mtu aliyeidhinishwa aliyetoa Amri hiyo lazima akague Amri hiyo mara moja baada ya kuitoa ili kuzingatia kama anapaswa kutoa 'Amri Inayoendelea ya Usalama wa Jumuiya' au kuighairi Amri. Maelezo zaidi kuhusu Amri Zinazoendelea yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo [hapa](#).

Unaweza kutoa wasilisho wakati wowote ili kueleza kwa nini ulitenda kwa njia fulani, jinsi itakavyoathiri wewe au mtoto wako au kitu kingine chochote anachohitaji kujua. Kwa mfano, unaweza kutaka kujulisha shule kwamba mtoto wako ana ulemavu ili iweze kuhakikisha kuwa unaweza kuendelea kumsaidia kwenda shule.

Wasilisho la maandishi linaweza kuwa barua pepe au barua kwa mtu aliyeidhinishwa. Unaweza kutumia kiolezo kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo [hapa](#).

Ikiwa hutaki kuandika wasilisho, unaweza kuomba kutoa wasilisho la mdomo badala yake. Unaweza pia kumwomba mtu mwingine atoe wasilisho kwa niaba yako, kama vile mtu anayekusaidia kwa ulemavu au mkalimani.

Je, nini kitatokea ikiwa sitafuata Amri?

Iwapo hutafuata sheria zilizowekwa katika Amri, shule inaweza kutuma maombi kwa Mahakama ya Hakimu ili kukufanya ufuate Amri hiyo.

Iwapo Mahakama ya Hakimu itaamua kwamba ulikosea kwa kutofuata Amri, inaweza:

- kukuhitaji ulipe faini
- kukuhitaji utii Amri
- kukuhitaji uchukue hatua mahususi ili kutii Amri hiyo
- kukuhitaji ufanye kitu kingine chochote ambacho Mahakama inadhani kinafaa.

Hutafungwa jela, wala kuandikishwa kwenye rekodi ya uhalifu au kupata adhabu ya uhalifu kwa kutofuata Amri.

Je, nifanye nini ikiwa nitahitaji huduma za utafsiri/ukalimani au usaidizi mwingine?

Ikiwa unahitaji mtafsiri, mkalimani au msaidizi, unaweza kumjulisha mwalimu mkuu wa shule ambaye anaweza kukusaidia kupata usaidizi huo.

Ikiwa mtoto wako anasomea shule ya serikali, unaweza pia kuwasiliana na ofisi ya eneo ya Idara ya Elimu na Mafunzo kwa usaidizi zaidi.

Kaskazini Mashariki mwa Victoria Simu: 1300 333 231 Barua pepe: nevr@education.vic.gov.au	Kaskazini Magharibi mwa Victoria Simu: 1300 338 691 Barua pepe: nwvr@education.vic.gov.au
Kusini Mashariki mwa Victoria Simu: 1300 338 738 Barua pepe: sevr@education.vic.gov.au	Kusini Magharibi mwa Victoria Simu: 1300 333 232 Barua pepe: swvr@education.vic.gov.au

Je, itakuwaje ikiwa ningependa kupata maelezo zaidi?

Unaweza kwenda kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo [hapa](#) kwa maelezo zaidi.